

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**  
TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA



Mtaa wa Kingalu

**S.L.P 845, 67109 MOROGORO**

Simu: 023-2614302

Nukushi: 023-2614478

Barua Pepe: [rbcmorogoro@pccb.go.tz](mailto:rbcmorogoro@pccb.go.tz)

Wavuti: [www.pccb.go.tz](http://www.pccb.go.tz)

**TAARIFA KWA UMMA KUPITIA VYOMBO VYA HABARI**

---

**JUNI 10, 2020**

**MEYA MSTAAFU NA WATAALAM WA ARDHI  
MBARONI KWA RUSHWA**

Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Mkoa wa Morogoro inaufahamisha Umma kwamba leo Jumatano, Juni 10, 2020 kwa kushirikiana na Ofisi ya Taifa ya Mashitaka itawafikisha mbele ya Mahakama ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Morogoro - Meya Mstaafu ambaye kwa sasa ni Diwani wa Kata ya Boma **Amir Juma Nondo** kwa makosa ya udanganyifu ambayo kwa mujibu wa marekebisho yaliyofanywa na Sheria Na. 3/2016 makosa hayo ni ya Uhujumu Uchumi.

Pamoja na Meya huyo watashtakiwa wengine ni:

- (ii) **Simon Michael Mahundo** aliyekuwa Afisa Mipango Miji,
- (iii) **Athumani Leonard Juma** aliyekuwa Mkuu wa Idara ya Mipango Miji na Mazingira Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro na
- (iv) **Dickson Steven Kesenha** ambaye alikuwa ni Afisa Mipango Miji wa Ofisi ya Katibu Tawala Mkoa wa Morogoro.

Tuhuma zinazowakabili watuhumiwa hao zinatokana na uchunguzi wa **TAKUKURU** mkoa wa Morogoro ambapo ilibainika kuwa Meya Mstaafu akiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Mipango Miji na Mazingira wa Halmashauri ya Manispaa Morogoro kwa kushirikiana na wataalam hao kwa mamlaka waliyokuwa nayo waliwasilisha taarifa za upotoshaji zilizosababisha mfanyabiashara mmoja wa mjini Morogoro kujipatia manufaa ya kubadili matumizi ya **kiwanja Namba 138 Kitalu D** kilichopo maeneo ya Msamvu B mjini Morogoro pasipo kufuata taratibu za Mipango Miji.

**TAKUKURU** Mkoa wa Morogoro inatoa **WITO** kwa viongozi wa kisiasa na watumishi wenye dhamana ya usimamizi wa Ardhi kuacha kabisa mazoea ya udanganyifu katika mchakato wa umilikishaji wa rasilimali Ardhi unaosababisha uwepo wa migogoro katika Mkoa wa Morogoro.

**TAKUKURU** haitasita kuwachunguza na kuwafikisha mbele ya Mahakama wale wote watakaobainika kujihusisha na vitendo hivyo.

Imetolewa na:

Janeth Machulya  
**Mkuu wa TAKUKURU (M)**  
**MOROGORO**